Namba ya Upimaji ya Mwanafunzi:.....

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE

04 HISABATI

Muda: 1: 30 Jumatano, 25 Oktoba, 2023 Asubuhi.

Maelekezo

1. Karatasi hii ina jumla ya maswali **Matano (05).**
2. Jibu Maswali yote.
3. Andika Namba yako ya Upimaji katika kila ukurasa sehemu ya juu upande wa kulia.

KWA MATUMIZI YA MPIMAJI TU		
NAMBA YA SWALI	**ALAMA**	**SAHIHI YA MPIMAJI**
1		
2		
3		
4		
5		
JUMLA		
SAHIHI YA MHAKIKI		


Namba ya Upimaji ya Mwanafunzi:.....

Na.	Swali	Sehemu ya Kazi	Jibu
1. (a)	Andika XLII kwa namba za Kiarabu		
(b)	Timu ya mpira wa miguu ya Masota ina miaka 22 tangu ianze. Andika miaka hiyo kwa namba za Kirumi.		
(c)	Andika 2020 kwa maneno		
(d)	Andika namba yenye makumi elfu 1, maelfu 7, mamia 4, makumi 1 na mamoja 3.		
(e)	Baba alilipa shilingi elfu tisa na hamsini kwa ajili ya ankra ya umeme. Andika kiasi hicho kwa tarakimu.		
2. (a)	Andika namba inayokosekana katika mfululizo ufuatao: 90, 85, 80, 75, ____, 65.		
(b)	) Ipi kubwa zaidi, 84×6 au 86×4 ?		


Namba ya Upimaji ya Mwanafunzi:.....

Na.	Swali	Sehemu ya Kazi	Jibu
(c)	Jaza namba inayokosekana katika mpangilio ufuatao: $\frac{1}{2}, \frac{1}{4}, _____, \frac{1}{16}$.		
(d)	Mgonjwa alipungua uzito kwa kg 1 kila mwezi. Ikiwa mwezi wa kwanza alikuwa na kg 90, je, mwezi wa sita alikuwa na uzito kiasi gani?		
(e)	Andika tendo lililotumika kupata mpangilio wa namba ufuatao: 99,89,79,69,59,49,39.		
3. (a)	Kitabu kina kurasa 91. Ikiwa kila ukurasa una picha 13, tafuta jumla ya picha zilizomo ndani ya kitabu hicho.		
(b)	Kokotoa $36x8 =$		
(c)	Jumlisha; Saa Dakika 14 30 + 8 40		
(d)	John alilala kwa muda wa saa 3 na dakika 45. Je, jumla alilala kwa dakika ngapi?		

Namba ya Upimaji ya Mwanafunzi:.....

Na.	Swali	Sehemu ya Kazi	Jibu
(e)	Toa; sh. 1980 – sh. 1300 =		
4. (a)	Mstatili una urefu wa sentimita 100 na upana wake ni sentimita 50. Nini mzingo wake?		
(b)	Andika jina la umbo lifuatalo:  		
(c)	Mstatili una mzingo wa sm 80 na urefu wa sm 25. Tafuta upana wake		
(d)	Uwanja wa mpira wa shule ya Mtakuja una mzingo wa m 480 na upana wa m 40. Tafuta urefu wake.		
(e)	Mzingo wa umbo la mraba ni sm 60. Tafuta urefu wa upande mmoja		

Namba ya Upimaji ya Mwanafunzi:.....

Na.	Swali	Sehemu ya Kazi	Jibu
5.	Soma takwimu katika picha ifuatayo inayoonesha mavuno ya shule, kisha jibu maswali yanayofuata:  Gunia 1 linawakilisha kg 1,000		
(a)	Mwaka gani shule ilipata mavuno mengi zaidi?		
(b)	Mwaka 2017 shule ilivuna kilogramu ngapi?		

Namba ya Upimaji ya Mwanafunzi:.....

Na.	Swali	Sehemu ya Kazi	Jibu
(c)	Mwaka gani shule ilipata mavuno machache zaidi ?		
(d)	Tofauti ya mavuno kati ya mwaka 2017 na 2015 ni kilogramu ngapi ?		
(e)	Mwaka upi shule ilikuwa na mavuno kg 6,000?		